



State of Michigan Attorney General Dana Nessel

KWA KUTOLEWA MARA MOJA:

Alhamisi Machi 26, 2020

Kutoka kwa Wakili Mkuu kwa Watu wa Michigan: Jua Haki Zako Za Kazini

LANSING – Idara ya Wakili Mkuu wa Michigan imeanzisha sehemu inayoitwa Jua Haki Zako za Kazi kwenye mtandao wa Idara hiyo ili kutoa habari na majibu kwa maswali yanayohusu haki za kisheria za wafanyakazi na waajiri chini ya Amri Kuu ya Utendaji ya Kaa Nyumbani, Kaa Salama iliyotolewa na Gavana Gretchen Whitmer, Wakili Mkuu Dana Nessel alitoa tangazo hili leo.

Mtandao huu pia unatoa habari kuhusu aina ya wafanyakazi wanaochukuliwa kuwa “wafanyakazi muhimu wa miundombinu” chini ya amri ya utendaji, ambao, kwa sababu hiyo, wanakubaliwa kufanya kazi nje ya nyumbani, na pia mtandao huo una maswali yanayouliziwa mara kwa mara kuhusu haki za mfanyakazi na majukumu ya mwajiri, na vitendo vilivyopendekezwa kwa askari walinda usalama na waendeshaji wa mashtaka.

Amri ya Kaa Nyumbani, Kaa Salama ilitolewa ili kupunguza kuenea kwa ugonjwa wa kirusi cha korona (COVID-19) na kulinda afya ya umma na ustawi wa wakazi wa jimbo la Michigan. Ukiukaji wa makusudi wa amri hii unaweza kusababisha faini ya \$500 na/au kifungo cha siku 90 cha jela kwa kila ukiukaji.

“Amri kuu ya utendaji na sheria nyingine za jimbo zinatoa ulinzi fulani kwa wafanyakazi wakati huu wa mabadiliko ya haraka kwenye mazingira, na ni muhimu kwa kila mkazi wa Michigan kuelewa haki zao,” alisema Nessel. “Bila shaka, janga hili linapoendelea, changamoto mpya na maswali mapya yatatokea, lakini tuna hakika kwamba hakuna kitu hatuwezi kushinda ikiwa tutafanyanya kazi kwa pamoja.”

Chini ya amri ya Gavana ya Kaa Nyumbani, Kaa Salama, kazi inayofanyiwa kazini kwa kawaida lakini isiyo ya lazima kwa kuendeleza au kulinda maisha ni marufuku. Isipokuwa mfanyakazi ameteuliwa na mwajiri wake kuwa mfanyakazi muhimu wa miundombinu, mfanyakazi huyo hawezi kulazimishwa kufanya kazi nje ya nyumbani. Ukiukaji wa makusudi wa amri hii ya utendaji ni makosa yanayofaa kuripotwa kwa askari walinda usalama wa sehemu ya utawala ambapo kosa hilo lilitendeka.

Zaidi ya hayo, sheria ya Michigan imekataza waajiri kubagua wafanyakazi wanaokutumia haki ambazo wanaweza kuwa wamepewa chini ya Sheria ya Usalama na Afya Kazini ya Michigan (MIOSHA). Kwa jumla, sheria ya Michigan inahitaji waajiri wahakikishe kila mfanyakazi ana, “mahali pa kazi ambapo hapajulikani kuwa na hatari zinazosababisha, au zina uwezekano wa kusababisha kifo au kuumia vibaya kwa mwili wa mfanyakazi.”

Ikiwa mfanyakazi anaamini kuwa mwajiri wake hafuatilii tahadhari sahihi kwa kuwalinda wafanyakazi kutoka kwa hatari mbalimbali, wanaweza kujifunza [jinsi ya kuwasilisha malalamiko kwa MIOSHA kwenye mtandao](#).

Muhtasari wa shughuli ambazo watu wanaweza kufanya na zile ambazo hawawezi kufanya chini ya amri kuu ya utendaji ya Kaa Nyumbani, Kaa Salama [yanaweza kupatikana hapa kwenye mtandao](#), [makala ya amri yanapatikana hapa](#) na majibu ya [maswali yanayoulizwa mara kwa mara kuhusu amri hii yanapatikana hapa](#).

Bonyeza hapa ili uone makala ya Wakili Mkuu ya [Jua Haki Zako za Kazi](#) kwenye mtandao.

Ofisi ya Wakili Mkuu itaendelea kupokea na kutathmini malalamiko ya wanunuzi kuhusu matukio ya kuongeza bei na kashfa, ingawa ukiukaji mwingine wa amri kuu za utendaji unafaa kuripotiwa kwa askari walinda usalama katika sehemu ya utawala ambapo kosa lililodaiwa lilitendeka. Malalamiko kuhusu matukio ya kuongeza bei yanaweza [kuripotiwa kwenye mtandao kwa timu ya Ulinzi wa Watumiaji ya Wakili Mkuu](#) au kwa kupiga simu nambari 877-765-8388.

Mtu yeyote anayetafuta tafsiri ya amri kuu ya utendaji anapaswa kwanza kuangalia amri hizo pamoja na maswali yanayoulizwa mara kwa mara yalitotajwa kwenye [mtandao wa jimbo uliotengwa kwa COVID-19](#). Viungo kuelekea kwa kurasa hizo za mitandao pamoja na taarifa za ziada zinaweza kupatikana kupitia kwa [mtandao wa Wakili Mkuu](#).

Kama jibu halitapatikani kwenye mtandao, ombi la tafsiri ya amri kuu linaweza kutumwa kupitia kwa [can Idara ya Wakili Mkuu ya Jimbo la Michigan](#).